**HOTUBA YA BIBI BENG'I M. ISSA, KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KATIKA KILELE CHA KONGAMANO LA NNE LA USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA MIRADI YA KIMKAKATI NA UWEKEZAJI LILILOFANYIKATAREHE 28 APRILI, 2024 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA BENKI KUU YA TANZANIA, DAR ES SALAAM**

Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu,

Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu;

Waheshimiwa Mawaziri;

Waheshimiwa Manaibu Waziri;

Mhe. Albert Chalamila , Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa;

Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu;

Ndugu Makatibu Wakuu wa Wizara,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Dar es Salaam,

Wakurugenzi wa Halmashauri za Dar es salaam,

Prof. Aurelia Ngirwa Kamuzora, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

Wajumbe wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi,

Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi,

Wawekezaji,

Wadau wa Maendeleo;

Wadhamini wa Kongamano;

Wawakilishi kutoka Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi;

Wawakilishi kutoka Taasisi za Elimu na Utafiti,

Wawakilishi kutoka Asasi za Kiraia,

Makampuni kutoka ndani na nje ya Nchi,

Wafanyabiashara,

Waratibu wa Uwezeshaji wa Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri mbalimbali;

Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana katika Kongamano la nne la Ushiriki wa Wananchi katika Uwekezaji na Miradi ya Kimkakati. Kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha Kongamano hili. Aidha, nawashukuru washiriki wote kutoka ndani na nje ya Jiji la Dar es salaam kwa kutenga muda wenu ili kushiriki katika Kongamano hili, Ushiriki wenu unaonesha dhamira ya dhati ya wadau mbalimbali kuwezesha watanzania kushiriki kikamilifu na kunufaika kutokana na uwekezaji na miradi ya kimkakati inayotekelezwa hapa nchini.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Nichukue nafasi hii ya kipekee kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji hapa nchini na kuhamasisha ushirikishwaji wa watanzania katika miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo imewezesha kuongeza ajira kwa watanzania, kupata masoko ya bidhaa na huduma kutoka kwenye kampuni za kitanzania na kujenga uwezo wa watanzania.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Kongamano hili la nne linawaleta pamoja wadau mbalimbali wanaohusika na masuala ya ushiriki wa watanzania katika uwekezaji na miradi ya kimkakati ili kubadilishana uzoefu pamoja na kujadili mada mbalimbali zinazohusiana na ushiriki wa watanzania (local content). Wadau wanaoshiriki katika Kongamano hili ni pamoja na viongozi wa Serikali ikiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri, Wawekezaji; sekta binafsi; taasisi za elimu na utafiti; wadau wa Maendeleo, wafanyabiashara, Asasi za Kiraia na Waratibu wa Madawati ya Uwezeshaji waliopo katika Wizara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri mablimbali. Lengo la Kongamano hili pamoja na masuala mengine ni:

a. Kujenga uelewa wa wadau mbalimbali kuhusu miradi ya kimkakati na uwekezaji inayotekelezwa hapa nchini;

b. Kushirikishana mafanikio na changamoto za ushiriki wa watanzania katika uwekezaji na miradi mbalimbali;
c. Kuwezesha sekta binafsi kufahamu fursa zilizopo kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa au inayotarajiwa kutekelezwa hapa nchini;
d. Kuwezesha wadau mbalimbali kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha ushiriki wa wananchi katika miradi mbalimbali;
e. Kuongeza uelewa wa wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa dhana ya local content katika uchumi wa nchi; na
f. Kuwezesha wadau mbalimbali kufahamiana na kujenga ushirika wa kufanya kazi pamoja katika masuala ya *local content*.

Tunatarajia baada ya Kongamano hili wadau watakuwa na ufahamu mkubwa wa miradi inayotekelezwa au inayotarajiwa kutekelezwa, sekta binafsi wataweza kuchangamkia fursa katika miradi mbalimbali na wadau mbalimbali watafahamu majukumu waliyo nayo katika kuongeza ushiriki wa watanzania katika uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeanza kuratibu masuala ya ushiriki wa watanzania katika uwekezaji na miradi ya kimkakati tangu mwishoni mwa mwaka 2015. Ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kufuatilia na kuratibu shughuli za ushiriki wa wananchi katika uwekezaji, Baraza limekuwa likifanya shughuli mbalimbali ikiwemo;

**a.** Kuunda kamati ya Taifa local content ya Sekta zote ambayo hukutana mara mbili kwa mwaka na kujadili masuala ya local content katika miradi na uwekezaji mbalimbali.

b. Kuunda kamati ndogo ndogo za ufuatiliaji wa local content katika miradi mahsusi mfano kamati ya local content ya mradi wa EACOP

c. Kuratibu makongamano ya local content tangu mwaka 2016 ambapo Kongamano lililopita lilifanyika mwaka 2021 hapa hapa Dar es Salaam.

d. Baraza pia limeunda mfumo wa uratibu wa masuala ya local content kwa kuwa na waratibu kwenye Wizara na Taasisi za Serikali zinazotekeleza au kusimamia miradi ya kimkakati na uwekezaji;

e. Kujenga uelewa kwa wadau mbalimbali kuhusu dhana ya Ushiriki wa Watanzania;

f. Kushirikiana na wadau katika kujengea uwezo wafanyabishara na kampuni za kitanzania ili kuziwezesha kushiriki katika fursa za miradi ya kimkakati na uwekezaji;

g. Kufanya tafiti bainifu pamoja;

h. Kutengeneza miongozo na;

i. Kufuatilia taarifa za ushiriki wa watanzania katika miradi na uwekezaji unaofanyika nchini na kutatua changamoto za ushiriki wao pale zinapojitokeza.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kauli mbiu ya Kongamano hili ni “**Wekeza Tanzania Kuongeza Thamani ya Ziada”**. Kauli mbiu hii imelenga kuhakikisha kuwa jitihada za makusudi zinafanywa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha uwekezaji unaongezeka ndani ya nchi ili kuweza kuongeza thamani ya ziada katika uchumi wa nchi. Kupitia uwekezaji watanzania wanapata fursa za ajira,

wanapata masoko ya uhakika wa bidhaa na huduma, wanaongeza ujuzi na uwezo wa kufanya kazi mbalimbali kupitia mafunzo na uhaulishaji wa teknolojia pamoja na jamii zinazozunguka maeneo ya uwekezaji kunufaika na huduma mbalimbali za kijamii, hivyo uwekezaji unapoongezeka nchini na thamani ya ziada nchini inaongezeka kwa wananchi na maendeleo nchini.

Tunaamini kwamba kadiri kampuni za ndani zinavyoshiriki kwenye uwekezaji na miradi ya kimkakati hapa nchini uwezo na ushindani wao unakua na hivyo utawezesha bidhaa na huduma za kitanzania kuweza kuwa na ushindani kikanda na kimataifa. Vilevile nguvu kazi ya kitanzania inapojengewa uwezo itawezesha watanzania kupata ajira ndani na nje ya nchi na hivyo kuwezesha kutekeleza malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mafanikio mbalimbali yamepatikana tangu Baraza lilipofanya Kongamano la kwanza la Ushiriki wa Watanzania mwaka 2016. Mafanikio hayo ni pamoja na:

- Kukua kwa uelewa wa wadau mbalimbali kuhusu dhana ya ushiriki wa watanzania;
- Sheria za sekta mbalimbali zinazingatia masuala ya ushiriki wa watanzania hasa katika sekta ya uziduaji (madini na petroli), fedha, bima, uwekezaji na ununuzi;
- Uzingatiaji wa utekelezaji wa masuala ya ushirikishwaji watanzania kwenye ajira, ununuzi na ujengaji uwezo kwenye uwekezaji na miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini; na

- Kuongezeka kwa ufuatiliaji na utoaji taarifa wa utekelezaji wa ushirikishwaji watanzania kwenye uwekezaji na miradi ya kimkakati.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Katika mwaka 2023 jumla ya idadi ya miradi ya ujenzi iliyotekelezwa ni 4,539 yenye thamani ya shillingi 8.5 Tn ikilinganishwa na miradi 4,012 yenye thamani ya shillingi 6.1 Tn iliyotekelezwa mwaka 2022. Idadi ya miradi iliyotekelezwa na wakandarasi wa ndani ilikuwa 4,404 yenye thamani ya shillingi 3.6 Tn na miradi iliyotekelezwa na wakandarasi wa kigeni ilikuwa ni 135 yenye thamani ya shillingi 4.9 Tn. Hivyo ushiriki wa wakandarasi wa ndani ulikuwa ni asilimia 97 na thamani ya miradi ni asilimia 42.4 huku ushiriki wa wakandarasi wa nje ulikuwa ni asilimia 3 na thamani ya miradi ilikuwa asilimia 57.6. Jitihada za uwezeshaji zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha makampuni ya kitanzania yanajengewa uwezo na yanaingia ubia wenye tija na kampuni kutoka nje ili kuwezesha thamani ya ziada kubwa kubaki hapa nchini ili kukuza sekta binafsi na uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Miradi ya kimkakati na uwekezaji ilizalisha ajira 162,968 za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 101,353 zilizozalishwa mwaka 2022 sawa na ongezeka la asilimia 37.8. Kati ya ajira zilizozalishwa mwaka 2023, ajira 156,661 zilikuwa za watanzania na ajira 6,307 zilikuwa za wageni. Vijana wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35 walifanikiwa kupata ajira 112,572 ambayo ni sawa na asilimia 69.1 ya ajira zote. Katika ajira zilizoenda kwa vijana, asilimia 70 walifanya kazi za ujuzi wa chini, asilimia 19 walifanya kazi za ujuzi wa kati na asilimia 11 walifanya kazi za ujuzi wa juu.

Kupungua kwa idadi ya ajira za wageni kunatokana na jitihada za makusudi za Serikali kuhakikisha watanzania wanashiriki na kunufaika na fursa za ajira kupitia mafunzo, urithishaji wa ujuzi na uhaulishaji wa teknolojia.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Katika kutekeleza miradi hii, Kampuni **3,360** za kitanzania zilipata fursa za kandarasi mbalimbali katika Miradi ya Kimkakati ikilinganishwa na kampuni **2,827** kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16. Aidha, idadi ya wakandarasi wa kitanzania waliosajiliwa ni **1,690** na wakandarasi walioingia ubia ni **64** katika kipindi cha mwaka 2023.

Bodi ya makandarasi imeendelea kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (*Contractors Assistance Fund – CAF*) kwa lengo la kuwasaidia makandarasi wa ndani kupata Dhamana za Zabuni (*Bid Security*) na Malipo ya Awali (Advance *Payment Guarantee*) kutoka katika Benki ya CRDB. Utaratibu huu umewezesha Makandarasi wa ndani kupata dhamana na hivyo kushiriki zabuni na kupata fedha za kuanzia kazi kwa urahisi. Mtaji wa mfuko huu (CAF) umefikia thamani ya TZS **4.1 Bilioni** kwa mwaka 2023 ukilinganisha na thamani ya **Bilioni 4.0** kwa mwaka 2022 ongezeko hili la mtaji linatokana na riba inayotolewa na benki katika fedha za mfuko huo ambazo zimewekwa kwa mfuko wa akaunti ya muda maalum (*Fixed deposit*).

Aidha, idadi ya wanachama wa mfuko imeongezeka kutoka **1,372** kwa mwaka 2022 hadi kufikia **1,411** kwa mwaka 2023. Ongezeko hili la wanachama linatokana na ongezeko la makandarasi wapya wanaosajiliwa na Bodi pamoja na ongezeko la shughuli za ujenzi katika mwaka 2023 kulinganisha na mwaka 2022. Aidha kwa mwaka 2023 jumla ya Makandarasi **190** walifaidika na mfuko huu kwa kupata dhamana zenye thamani ya TZS **11.8 Bilioni**.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Tumeanza Kongamano hili siku ya jana 27/4/2024 ambapo Taasisi mbalimbali zinazosimamia miradi ya Kimkakati na Uwekezaji unaofanyika kwenye sekta mbalimbali ziliwasilisha mawasilisho na mijadala mbalimbali ikiwemo kujadili mafanikio yaliyopatikana kwenye masuala mbalimbali yakiwemo ya ajira, ununuzi, mafunzo na huduma kwa jamii na kutoa mapendekezo mbalimbali ambayo sisi kama waratibu tumeyachukua na kufuatilia utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado kuna changamoto ambazo zinakabili nguvu kazi na kampuni za kitanzania kushiriki kwenye uwekezaji na miradi ya kimkakati ikiwemo kukosa ithibati za kimataifa, mitaji midogo pamoja na kuwa na uwezo mdogo  wa kuzalisha bidhaa kwa wingi. Hivyo, Baraza pamoja na wadau mbalimbali wameendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuondoa changamoto hizo ikiwemo kutoa mafunzo, kuboresha ubora wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na kutengeneza bidhaa za kifedha zakuwezesha kampuni za kitanzania kuongeza mitaji yao.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kipekee napenda kushukuru Taasisi zilizoshirikiana na Baraza katika kuandaa kongamano hili ambapo kwanza napenda kutambua mchango wa muandaaji mwenza wa Kongamano hili ambae na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA). Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Mgeni Rasmi naomba nimuite Mkuu wa Taasisi ya PURA, Eng. Charles Sangweni aje atoe salamu zake kwa ufupi.

Pia  Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wote ambao wamejitoa kwa hali na mali ili kuhakikisha Kongamano hili linafanyika. Taasisi hizo ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), TradeMark Africa, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Chuo cha Mipango Dodoma (IRDP), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Benki ya Azania, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Dar es Salaam Institute of Technology (DIT), Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) pamoja na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (ERB). Tunashukuru sana kwa michango yenu katika kufanikisha Kongamano hili.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mwisho kabisa napenda kuwakaribisha wadau mbalimbali kushirikiana na Baraza katika kuwezesha watanzania kushiriki kikamilifu na kunufaika na uwekezaji na miradi ya kimkakati inayotekelezwa hapa nchi ili kuinua uchumi wa mtu moja moja na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Naomna Kuwasilisha na;

Asanteni kwa kunisikiliza.